Diaspora Council of Tanzanians in America

Februari 20, 2021

Buriani Mh. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar

Taasisi ya Diaspora Council of Tanzanians in America (DICOTA) imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kilichotokea Februari 17, 2021 katika hospitali ya Taifa ya Muhumbili jijini Dar es Salaam.

Uongozi wa DICOTA, pamoja na wanachama wa DICOTA, tunatoa salamu za pole kwa wananchi wote wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba huu mkubwa kwa Taifa letu. Tunatoa pia pole za kipekee kwa ndugu wote na familia ya marehemu.

Katika kipindi cha uhai wake, Mh. Maalim Seif amekuwa nguzo muhimu ya ujenzi wa demokrasia Tanzania na mtetezi mkubwa wa maslahi ya Zanzibar. Hakika Taifa letu limepoteza kiongozi Mzalendo na Shupavu, aliyeonyesha ujasiri wa pekee kwa kutamka wazi maambukizi yake binafsi ya Uviko-19 (Covid-19). Marehemu alituasa tuendelee kuchukua tahadhari dhidi ya mlipuko wa Uviko-19 (Covid-19), ikiwa ni pamoja na kuvaa barakoa, kuosha mikono kwa maji tiririka na kuepeuka mikusanyiko ya watu wengi.

Aidha, DICOTA ingependa kuona mipango na juhudi madhubuti za kuidhinisha na kufikisha chanjo za Uviko-19 (Covid-19) Tanzania ili kuongeza kinga kwa wananchi wa Zanzibar, na kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla.

Kwa niaba ya DICOTA tunafikisha salamu hizi za rambirambi kwa wananchi wa Zanzibar, wa Tanzania bara na pia kwa familia ya marehemu.

“INNA LILLAHI WA INNA ILAYHII RAAJI’UN. HAKIKA SISI NI WA MWENYENZI MUNGU NA HAKIKA SISI KWAKE NI WENYE KUREJEA”

Dkt. Frank Minja
Rais, DICOTA

Bi. Asha Nyang’anyi
Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, DICOTA